





# Demokrasia, udikteta na maandamano:

## Wananchi wanasemaje?

## 1. Utangulizi

Japokuwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli imejipatia pongezi nyingi kwa jitihada zake za kupambana na utendaji mbovu na usio wa ufanisi, pamoja na vitendo vya rushwa, pia imekuwa ikikosolewa kuhusu mtazamo wake katika masuala ya kidemokrasia na haki za binadamu. Vyombo vya habari, bunge na vyama vya upinzani vimewekewa vizuizi vingi vipya vinavyozuia utekelezaji wa shughuli zao. Vitendo kama vile kuzuia kurushwa kwa matangazo ya moja kwa moja ya bunge, kufungiwa kwa baadhi ya vyombo vya habari, kufikishwa mahakamani kwa Watanzania sita kwa madai ya kumtukana Rais na kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara ya kisiasa vimegusa hisia za wananchi wengi. Mnamo tarehe 7 mwezi Juni mwaka 2016, jeshi la polisi lilitoa zuio kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara. Baadae, Rais Magufuli alisema hakuna uchaguzi uliopangwa hadi hapo mwaka 2020, hivyo mikutano hiyo itapunguza umakini kwa serikali na wananchi katika jitihada za kuleta maendeleo.

Kwa upande wa vyama vya upinzani, vizuizi hivo vilichukuliwa kama ukiukwaji wa haki zao za kikatiba na za kidemokrasia za uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kutoa maoni. Baadhi yao walimwelezea Rais Magufuli kama “dikteta”. Viongozi wa Chadema, walianzisha Umoja wa Kupinga Udikteta Tanzania (UKUTA) – na kuitisha maandamano nchi nzima yaliyopangwa kufanyika tarehe 1 Septemba, 2016. Serikali ilipokea kitendo hicho kama tishio la amani na polisi wakakataa kutoa kibali cha maandamano hayo. Viongozi wa UKUTA walielezea kuwa huo ni ukiukwaji mwingine wa haki zao, na kusisitiza kuwa wamepanga kuendelea na maandano hayo, hata bila ruhusa ya polisi.

Muhtasari huu umebeba maoni ya wananchi kuhusu demokrasia, udikteta na maandamano nchini Tanzania. Je, wananchi

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 |
Bp: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

wanakubaliana na mtazamo unaosema kwamba Rais ni dikteta? Nini maoni yao kuhusu demokrasia ya vyama vingi na uhuru wa kutoa maoni? Je, wanaunga mkono maandamano ya UKUTA? Na je, wana mpango wa kushiriki?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* ikiwa ni moja ya programu za Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana katika tovuti yetu kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu zimekusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,602 kutoka kundi la pili la *Sauti za Wananchi*. Waholjiwa walipigiwa simu kati ya tarehe 24 na 29 Agosti mwaka 2016. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania bara pekee.

Maoni ya muhtasari huu yalikusanywa wakati ambapo baadhi ya wanasiasa, wasomi na wanazuoni walikuwa wamepanga kufanya maandamano tarehe 1 Septemba. Polisi walikua bado wamekataa kuyaruhusu maandamano hayo. Tarehe 31 Agosti, baada ya takwimu kukusanywa, viongozi wa Chadema walitangaza kusitisha maandamano kwa muda mpaka tarehe 1 Oktoba, ili kutoa muda zaidi kwa madai yao kushughulikiwa kwa njia ya mazungumzo.

Muhtasari huu unajumuisha maoni ya wananchi yaliyochambuliwa kulingana na ufuasi wa vyama vya siasa. Ufuasi huu ulibainika kwa kuwauliza swali la “je, ni chama gani ulicho karibu nacho zaidi?” Asilimia 66 waliripoti kuwa karibu na chama tawala (CCM), wakati asilimia 19 wakisema walikuwa na ukaribu na vyama vya upinzani. Kati ya wale waliokaribia upande wa vyama vya upinzani, asilimia 16 walitaja ukaribu wao kuwa kwa Chadema, na asilimia 3 walitaja vyama vingine. Asilimia 15 waliripoti kutokuwa na ukaribu na chama chochote.

Matokeo muhimu ni:

- Wananchi saba kati ya kumi wanaunga mkono demokrasia kama mfumo bora wa serikali, mtazamo huu unafanana miongoni mwa wafuasi wa vyama mbalimbali.
- Uungaji mkono wa shughuli za upinzani baada ya uchaguzi umepata maoni tofauti tofauti, lakini uungaji mkono uhuru wa kutoa maoni ni mkubwa.
- Mwananchi mmoja kati ya watatu alitoa maana kuhusu neno ‘udikteta’, akilitafsiri kama serikali kutumia nguvu wakati wa kuitawala nchi.
- Mwananchi mmoja kati ya kumi anasema Tanzania kwa sasa inaongozwa na ‘dikteta’.
- Wananchi sita kati ya kumi wanaunga mkono uzuiaji wa mikutano ya vyama vya siasa katika kipindi kisicho cha kampeni za uchaguzi.
- Asilimia 16 wanafamu UKUTA. Uelewa kuhusu harakati hiyo ni mkubwa miongoni mwa wale wanaofahamu harakati hizo.
- Vile vile, asilimia hamsini ya wafuasi wa Chadema wanaunga mkono harakati za UKUTA na asilimia kumi na moja ya wafuasi wa CCM wanaunga mkono harakati hizo.
- Hadi hapo utafiti huu ulipokuwa unafanyika, wananchi watatu kati ya kumi walisema wapo tayari kushiriki kwenye maandamano yoyote ambayo yanaendana na mitazamo yao. Wananchi watatu kati ya kumi wanasema wapo tayari kushiriki kwenye maandamano yoyote ambayo yanaendana na mitazamo yao
- Mwananchi mmoja tu kati ya kumi aliyepanga kushiriki kwenye maandamano ya UKUTA.


# 2. Mambo tisa kuhusu maoni ya wananchi juu ya demokrasia

## Jambo la 1: Wananchi saba kati ya kumi wanaikubali demokrasia kama mfumo bora wa utawala

Asilimia 69 wanaielezea demokrasia kama mfumo unaokubalika zaidi kuliko aina nyingine za mifumo ya serikali huku asilimia 16 wakisema kuwa kuna nyakati ambazo utawala usio wa kidemokrasia unaweza ikakubalika.

Katika mitazamo yote, matokeo yao yanaendeana na maoni ya wafuasi wa vyama vyote.[1]

**Kielelezo cha 1: Je, ni kauli gani kati ya hizi kuhusu demokrasia inakaribiana na mtazamo wako?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)
*Asilimia zinaweza zisifike 100% kutokana na makidirio*

## Jambo la 2: Uwepo wa vyama vingi unaungwa mkono na walio wengi, lakini wananchi wamegawanyika kuhusu shughuli za kisiasa katika kipindi kisicho cha kampeni

Asilimia 80 ya wananchi wanasema kwamba baada ya uchaguzi, juhudi za kimaendeleo zipewe kipaumbele na vyama vya siasa. Kwa upande mwingine asilimia 86 ya wananchi wanasema Tanzania inahitaji vyama vya upinzani ili wananchi waweze kuchagua vema nani wa kuwaongoza. Kuhusu mchango wa mikutano ya vyama vya upinzani baada ya vipindi vya uchaguzi, wananchi wamegawanyika katikati. Asilimia 51 wanasema mikutano husaidia kuiwajibisha serikali na huchangia maendeleo, lakini asilimia 49 wanasema mikutano huvuruga umakini wa serikali na wananchi, na kudhoofisha shughuli za kimaendeleo.

1 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)


**Kielelezo 2: Maoni juu ya shughuli za vyama vya upinzani:**
**Kauli gani unakubaliana nayo zaidi?**




**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)

Asilimia 95 – wakiwemo wafuasi wa chama tawala na vyama vya upinzani – wanaunga mkono haki ya wananchi kuikosoa serikali. [2]

**Kielelezo cha 3: Maoni kuhusu haki za kidemokrasia:**
**Asilimia ya wananchi wanaokubali na mitazamo ifuatayo:**





**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)

2 ibid

## Jambo la 3: Mwananchi mmoja kati ya watatu alitoa maana ya neno “udikteta” akilitafsiri kama kutawala kimambavu.’

Wananchi wana uelewa tofauti tofauti kuhusu neno “udikteta”, lakini mwananchi mmoja kati ya watatu (asilimia 32) analitafsiri kama kutawala kimabavu. Asilimia 15 wanalitafsiri neno hilo kama mtu mmoja ndiye mwenye maamuzi nchini. Hatahivyo, asilimia 34 wanasema hawaelewi nini maana ya neno hilo.[3]

**Kielelezo cha 4: Je, neno udikteta lina maana gani kwako?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)

## Jambo la 4: Asilimia 11 wanaamini Tanzania inaongozwa na dikteta, huku asilimia 58 wakipinga


Baadhi ya wanasiasa na wasomi wanautafsiri uongozi wa Rais Magufuli kama udikteta, na neno hilo likiwa mmojawapo wa maneno yanayounda UKUTA. Asilimia 11 ya wananchi wanakubaliana na wazo hilo lakini asilimia 58 wanalipinga. Asilimia 31 wanasema hawana uhakika.

Makundi tofauti tofauti katika jamii yana maoni kadhaa kuhusu suala hili. Asilimia 13 ya wanaume wanamuita Rais dikteta huku asilimia 8 ya wanawake wakimuita hivo. Makundi ya vijana, matajiri na wenye elimu ya juu wanamuona Rais dikteta kuliko wazee, masikini na wenye elimu ya chini.

Utofauti mkubwa unaonekana pale tunapoangalia iwapo kuna utofauti wa maoni kati ya vyama vya siasa. Asilimia 29 ya wananchi walio karibu karibu na vyama vya upinzani wanamwona Rais Magufuli kama dikteta. Miongoni mwa wale ambao wanajiona wapo karibu na chama tawala, asilimia 5 wana mtazamo huo, ikimaanisha kuwa mmoja kati ya wafuasi ishirini wa CCM wanamwona mwenyekiti wa chama kama dikteta.[4]

3 ibid
4 ibid

**Kielelezo cha 5: Je, unadhani Tanzania inaongozwa na dikteta?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)
*Asilimia zinaweza zisifike 100% kutokana na makidirio*


## Jambo la 5: Wananchi watatu kati ya kumi wanasema wapo tayari kushiriki kwenye maandamano

Aslimia 29 wanasema wana uwezekano mkubwa wa kushiriki kwenye maandamano yoyote yale iwapo "kuna jambo ambao haliwafurahishi" huku asilimia 50 wakisema hakuna uwezekano wa wao kushiriki kwenye maandamano yoyote. Vijana wanaonesha utayari wa kushiriki katika maandamano kuliko wazee.

Miongoni mwa waliosema wangeweza kujiunga na maandamano, asilimia 95 wanayaone maandamano kama njia ya "kutafuta haki/kupinga jambo/kuonyesha tatizo kwenye jamii."

Miongoni mwa wale waliosema hawatajiunga na maandamano, asilimia 45 wanasema ni kwa sababu wana wasiwasi itatokea vurugu, na asilimia 29 kwa sababu "siyo njia sahihi ya kutatua matatizo."[5]

**Kielelezo cha 6: Utayari wa kujiunga kwenye maandamano**




**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)
*Asilimia zinaweza zisifike 100% kutokana na makidirio*


## Jambo la 6: Wananchi sita kati ya kumi wanaunga mkono kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa, akiwemo mfuasi mmoja kati ya watatu wa vyama vya upinzani

Asilimia 60 wanaunga mkono maamuzi ya Rais ya kuzuia mikutano ya hadhara ya kisiasa. Uungwaji mkono huo ni mkubwa (asilimia 70) miongoni mwa wafuasi wa chama tawala na ni mdogo (asilimia 31) miongoni mwa wafuasi wa vyama vya upinzani. Pamoja na hayo, wazee wengi zaidi wanaunga mkono uamuzi huo (asilimia 70) kuliko vijana (asilimia 55).

Hata hivyo, wafuasi wa kila chama wanapingana na uongozi wa vyama vyao kwenye suala hili: asilimia 31 ya wafuasi wa vyama vya upinzani wanakubaliana na kuzuiwa kwa maandamano ya UKUTA.[6]

5 ibid
6 ibid

**Kielelezo cha 7: Je, unakubaliana na maamuzi ya kuzuia mikutano ya vyama vya siasa?**





**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)
*Asilimia zinaweza zisifike 100% kutokana na makidirio*


## Jambo la 7: Mwananchi mmoja kati ya sita anaufahamu UKUTA, na uelewa wake ni mkubwa miongoni mwa hao wanaofahamu

Asilimia 16 wanafahamu harakati za UKUTA, huku asilimia 79 wakiwa hawafahamu harakati hizo. Miongoni mwa wale wanaofahamu UKUTA, uelewa wao kuhusu harakati hizo ni mkubwa; kwa usahihi wameelezea UKUTA kama; Umoja wa Kupinga Udikteta (asilimia 48), upinzani wanaotetea haki zao (asilimia 20) na kupinga serikali (asilimia 8). Vilevile, miongoni mwa wanaofahamu UKUTA, asilimia 84 waliijua siku iliyopangwa kwa ajili ya maandamano.[7]

**Kielelezo cha 8: Uelewa kuhusu UKUTA**




**Kielelezo cha 9: Ufahamu kuhusu UKUTA (Miongoni mwa wanaoelewa UKUTA)**





**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)

7 ibid

## Jambo la 8: Mwananchi mmoja kati ya watano anaunga mkono harakati za UKUTA, ikiwemo nusu ya wafuasi wa vyama vya upinzani

Asilimia 22 ya waliohojiwa walifahamu kuhusu UKUTA na waliripoti kuiunga mkono. Uungwaji mkono wa UKUTA ulikuwa juu zaidi kwa wafuasi wa vyama vya upinzani. Lakini kundi hili liligawanyika pasu kwa pasu, asilimia 50 wakisema wanaiunga mkono UKUTA wakati asilimi 44 wakisema hawaiungi mkono. Asilimia 6 ya wafuasi wa chama tawala wanaiunga mkono UKUTA.

**Kielelezo cha 10: Uungaji mkono UKUTA (Kati ya wananchi waliokuwa wanaifahamu)**





**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)
*Asilimia zinaweza zisifike 100% kutokana na makidirio*

## Jambo la 9: Mwananchi mmoja kati ya kumi alipanga kushiriki kwenye maandamano ya UKUTA ya Septemba 1

Miongoni mwa wale waliokuwa wakifahamu harakati ya UKUTA, asilimia 9 kati yao walipanga kushiriki maandamano ya Septemba 1. Hii ilikuwa ni pamoja na asilimia 24 ya wafuasi wa vyama vya upinzani, na asilimia 3 ya wafuasi wa chama tawala.

**Kielelezo cha 11: Walioonyesha uwezekano wa kushiriki katika maandamano ya UKUTA Septemba 1 (Kati ya wananchi waliokuwa wanaifahamu)**




**Chanzo cha Takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 12 (Septemba 2016)

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu umewasilisha matokeo anuwai kuhusu mitazamo ya wananchi juu ya demokrasia na uhuru wa kutoa maoni. Kwa undani zaidi, takwimu zinaonyesha kuwa wananchi wana mitazamo mchanganyiko na inayokinzana kuhusu nchi inavyoongozwa.

Suala la amani na utulivu nchini Tanzania limejengeka katika fikra za Watanzania kwa miaka mingi sasa. Katika muktadha huo, chama tawala kinaonekana kuwa kimejenga imani kwa wananchi walio wengi kuwa vitendo vyovyote vya kudai haki vinaweza kuleta uvunjifu wa amani nchini. Hii inaweza kusababisha wananchi kutoshiriki maandamano na harakati za kudai haki za kidemokrasia.

Mtazamo huu unajidhihirisha kwenye mgawanyiko uliopo miongoni mwa maoni ya wananchi kuhusu wajibu wa vyama vya upinzani baada ya uchaguzi. Hii inajitokeza pale ambapo nusu ya watanzania wanasema kuwa upinzani uwe na jukumu la kuchangia maendeleo endelevu na asilimia kubwa wanakubaliana na kuzuiwa kwa maandamano na mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Wakati huo huo idadi kubwa ya wananchi wanaunga mkono uhuru wa kutoa maoni na haki yao ya kuikosoa serikali.  Na pia wanaunga mkono demokrasia bila wasiwasi.

Harakati za UKUTA zimepata viwango hivi vya uungwaji mkono na kufahamika katika kipindi kifupi sana cha chini ya miezi miwili. Idadi hii inaweza kuonekana ndogo, lakini ni kubwa kutokana na muda mfupi wa maandalizi na pia ikizingatiwa kwamba serikali ya awamu ya tano inakubalika na wananchi walio wengi.

Takwimu hizi zinaendana na zile za mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now), zikionesha kuwa asilimia 16 wanafamu kuhusu mpango huu, pamoja na kwamba mpango huu umeshadumu kwa zaidi ya miaka mitatu.[8]

Kwa ujumla, mfumo wa kidemokrasia, uwepo wa vyama vingi na uhuru wa kutoa maoni unaungwa mkono na wananchi walio wengi. Lakini wengi pia hawakubaliani na mbinu zinazotumiwa na baadhi ya viongozi wa upinzani katika kuhakikisha demokrasia inalindwa.

Matokeo haya yana maana kubwa na pana. Mfuasi mmoja wa CCM kati ya ishirini anasema mwenyekiti wa chama chake ni dikteta. Idadi inayofanana na hiyo inaunga mkono harakati ya UKUTA na kupanga kushiriki maandamano ya Septemba 1. Pia, wafuasi wa vyama vya upinzani wanaounga mkono wazo la serikali kutofuata demokrasia katika baadhi ya mambo ni wengi kuliko wafuasi wa chama tawala.

Katika muktadha huu, mfuasi mmoja kati ya watatu wa vyama vya upinzani anakubaliana na kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, na nusu ya wafuasi hao hawaungi mkono harakati za UKUTA. Upande mwingine, robo tatu ya wafuasi wa chama tawala wanaunga mkono haki ya kufanya mikutano ya siasa baada ya uchaguzi, tofauti na msimamo wa mwenyekiti wa chama chao na Rais wa nchi.

8 *Sauti za Wananchi* Mobile Phone Survey – Round 17 of first panel (July 2014)

Ifahamike kuwa mwananchi mmoja kati ya sita amesikia kuhusu harakati za UKUTA, na moja kati ya watano anaunga mkono harakati hiyo.. Haya ni mafanikio makubwa kwa harakati za UKUTA ambazo hazikuwepo mwezi Juni 2016. Pamoja na hayo, idadi kubwa ya watanzania hawakubaliani na maelezo ya vyama vya upinzani kuwa Rais Magufuli ni dikteta.

Matokeo haya ni ishara ya changamoto kwa upande wa upinzani wakati wa kuandaa harakati zinazolenga kuikosoa na kuiwajibisha serikali.

Kwa upande wa serikali na chama tawala, uungwaji mkono wa demokrasia ya vyama vingi na uhuru wa kutoa maoni vinafaa kuzingatiwa. Japokuwa idadi kubwa ya Watanzania kwa sasa hawakubali kuwa Rais Magufuli ni dikteta, matokeo ya utafiti huu unaonyesha kuwa hatua za ziada za kuudhibiti uhuru wa kutoa maoni na kukusanyika havitapokelewa vizuri. Wananchi wanasema baadhi ya vizuizi kwenye haki za kidemokrasia ni muhimu ili kulinda amani na kuharakisha maendeleo lakini iwapo vitendo visivyo vya kidemokrasia vitafika mbali zaidi, utayari wao wa kukubaliana navyo huenda ukabadilika.

Siyo wapinzani wala chama tawala ambao wapo tayari kupuuzia maoni ya wafuasi wao na ya wananchi kwa jumla. Pia ni vema serikali ikapokea na kuzingatia maoni ya wananchi yanayohusu utendaji wake. Hata kama maamuzi yana malengo mazuri, wananchi wanapenda taratibu za kidemokrasia zizingatiwe katika utekelezaji wa maamuzi hayo.